

SHULE YA SEKONDARI NATA,
S.L.P 503,
NATA-NZEGA
Mob 0782306457

Tarehe.....

JINALAMWANAFUNZI.....
S.L.P.....
NZEGA.

YAH:MAAGIZO YAKUJIUNGA NASHULE YASEKONDARI NATA.
WILAYA YA NZEGA MKOA WA TABORA,MWAKA2021.

1.0UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifukwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka2021.Shule ya sekondari **Nata** ipo umbali wa km 97 kutoka Makao makuu ya wilaya,muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe11/01/2021 Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe11/01/2021 namwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021ndani ya siku saba.

2.0MAMBOMUHIMUYAKUZINGATIA

2.1Sare za shule

- a) suruali rangi ya damu ya mzee na shati rangi nyeupe mikono mifupi kwa wavulana na kwa wasichana sketi rangi ya damu ya mzee linda box mbele na nyuma na shati rangi nyeupe mikono mirefu, sketi iwendefu hadi usawa wa soksi.
- b) Rangi ya ljabu iwe ni rangi nyeupe (muislamu pekee), mzazi atanunua mwenyewe nyumbani.
- c) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suit nyeusi kwa wote .
- d) Sweta na tai rangi ya damu ya mzee kwa wote .
- e) T-shirt kwa wote ni rangi ya blue(Maelekezo ya T-shirt utayakuta shuleni.
- f) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kamba soksi za rangi nyeupe kwa wote.

2.2 Daftari za kawaida nne(4) na daftari kubwa(counterbook quire 2) 9,Dictionary,kalamu na mkebe (mathematical set) Mzazi atanunua mwenyewe.

3.0 SHERIANAKANUNIMUHIMUZASHULE

Shule inaendeshwa kwamujibu wa sharia Na.25 ya Elimu ya mwaka1978 kama Iliyorekebisha kwa sheriaNa.10 yamwaka1995.Aidha inazingatia miongozo Yote ina yotolewa na OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo lalazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shuleni lazima.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote na wanafunzi wenzako.
- e) Kuzingatia usafi wa mwili,mavazi na mzingira ya shule.
- f) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

- g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa na
- h) Kutunza mali zaUMMA.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWASHULE.

- a) wizi.
- b) Uasherati.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevinamatumiziyamadawyakulevyakamavileuvutajiwabangi,cocaine, mirungi,kuberin.k
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi malizaUMMA.
- g) Kuwamjamzito/kupatamimba
- h) Kuoja/kuolewa.
- i) Kudharau bendera yaTaifa
- j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki katika kuvuruga amani na usalamawashuleauwatu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE YA MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWASHULENINAMWANAFUNZI.

- a) Medical examination form.Ambayo itajazwa naMgangaMkuuwa Hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa Kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomuya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelezo mengine Yatakayo tolewa na shule.
- d) Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNISANAKATIKASHULEHII WAKO

.....

MATHIAS.E.MPYA

MKUUWASHULE